Ili kurahisisha utengenezaji wao, Prof Kamau alitoa wito kwa serikali kubuni sera zinazosaidia kutumiwa kwa magari ya umeme na kuhakikisha kuondolewa kwa ushuru wa vipuri ikiwa ni pamoja na chuma, betri na vifaa vingine.



Prof Gitau Kamau, mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Zitech aonyesha tuktuk inayotumia umeme ambayo amevumbua.

Miundombinu ya maji ya Sh77m kuinua usambazaji katika Makueni



Mradi wa Maji wa Athi-Kilema-Tunguni uliozinduliwa na Gavana Mutula. Picha na Patrick Nyakundi

NA PATRICK NYAKUNDI (KNA)

Gavana wa Makueni Mutula Kilonzo Jr. amezindua miradi mitatu ya maji yenye thamani ya zaidi ya Sh77 milioni katika Wadi ya Kikumbulyu Kaskazini, ambayo inatazamiwa kunufaisha takriban watu 111,000.

Katika eneo la Kiaoni, Mutula alikuwa upanuzi wa bomba la maji la Makeni-Kiaoni kwa kilomita 4.4. Mradi huu ulijumuisha ukarabati wa kibanda cha Maji cha Kiaoni, kuinuliwa kwa mnara wa tanki, na uwekaji wa tanki la mita za ujazo 10 kwa gharama ya Sh4.3 milioni.

Vile Vile, Mkuu wa kaunti alizindua tanki la kuhifadhi maji lenye uwezo wa mita za ujazo 225,000 lililojengwa na Kampuni ya Maji ya KIBMASCO eneo la Kathyaka kwa gharama ya Sh4.5 milioni. Tanki hili lita-hudumia watu 6,300 katika maeneo ya Ngulu na Nyayo.

“Kuzinduliwa kwa miradi hii ya maendeleo ya maji kunalenga kuhakikisha upatikanaji wa maji salama na ya kutosha katika Kaunti ya Makueni kwa matumizi ya maji jumbani, unyunyuzaji na viwandani,” alisema Mutula

**Miradi hii
ya maji
inalenga
kuhakikisha
upatikanaji wa
maji salama na
ya kutosha**

katika soko la Kiaoni wakati wa kuzindua mradi wa maji wa Makeni-Kiaoni.

Huko Athi, Gavana alizindua mradi wa maji wa Athi-Kilema-Tunguni, ambao umegharimu Sh68 milioni. Mradi huu unatarajiwa kunufaisha zaidi ya watu 100,000 katika wadi za Kikumbulyu Kaskazini, Makindu, na Nguumo.

Miongoni mwa wigo wa kazi hizo ni pamoja na ujenzi wa tanki la maji lenye urefu wa mita za ujazo 250,000 katika kilima cha Mukononi na mifumo ya kielektroniki ya mitambo ya kuweka dawa kusafisha maji, mitandao ya usambazaji maji kwa wadi za Makindu, Kikumbulyu Kaskazini na Nguumo na ujenzi wa vioski vinne vya maji.

Kazi nyingine ni pamoja na uwekaji wa paneli tatu za Wati 100 za sola, taa za barabarani, uwekaji wa pampu ya kuingiza kemikali na kupaka rangi sehemu za tanki zilizo-inuliwa na ukarabati wa baadhi ya vifaa.

Katika ziara hiyo, Mutula pia alizindua miradi miwili ya chekechea (ECDE) ambapo madarasa na vyoo vitatu na ofisi zilijengwa kwa Sh7 milioni.

Katika vituo vya ECDE vya Kyaani na Katilani, madarasa mawili, ofisi na vyoo vitatu kwa kila moja vilijengwa.

“Serikali yangu imeanza kuhakikisha wanafunzi wa ECDE wanajifunza katika mazingira mazuri na yanayofaa,” alisema Mutula alipokuwa akizindua miradi hiyo.



KENYA UNIVERSITIES AND COLLEGES CENTRAL PLACEMENT SERVICE (KUCCPS)

KENYA MEDICAL TRAINING COLLEGE SEPTEMBER 2024 INTAKE

The Kenya Universities and Colleges Central Placement Service (KUCCPS) invites applications for placement in various programmes offered at the Kenya Medical Training College (KMTc) for the September 2024 intake. Applications must be submitted through the KUCCPS Student's Portal students.kuccps.net.

Available Programmes

Available programmes, minimum subject requirements and KMTc campuses are listed below.

S/No.	Programme Name	Minimum Requirements	KMTc Campuses
1.	Certificate in Medical Engineering	Minimum Mean Grade: C- Minimum Subject Requirements: Eng / Kis : C- Mat A: D Phy / Psc: D- Bio / Che / Bsc / Mw / Ect / Drd: D	Bomet, Embu, Kilifi, Kisii, Kisumu, Lake Victoria, Loitokitok, Makindu, Meru, Nairobi
2.	Diploma in Health Records and Information Technology	Minimum Mean Grade: C Minimum Subject Requirements: Eng / Kis : C Mat A: C- Bio / Bsc: D+ Phy / Che / Psc / Geo / Econ / Hsc / Agr / Cmp / Com / Bst: C-	Bondo, Isiolo, Meru - Maua Satellite, Siaya
3.	Certificate in Orthopedic Trauma Medicine	Minimum Mean Grade: C- Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: C- Bio / Bsc: C- Mat A / Phy / Che / Psc / Hsc / Agr / Ww / Mw / Drd / Cmp: D+	Busia, Garissa, Kangundo, Kapenguria, Kaptumo, Makindu, Makueni, Mbooni, Meru - Mithene Satellite, Muranga, Mwingi, Port Reitz, Shianda - Mumias, Siaya, Sigowet, Trans-Mara, Vihiga, Voi, Kakamega - Navakholo
4.	Certificate in Health Records and Information Technology	Minimum Mean Grade: C- Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: C- Bio / Bsc: D Mat A: D- Phy / Che / Psc / Gsc / Geo / Econ / Hsc / Agr / Cmp / Com / Bst: D+ : D- Phy / Che / Psc / Gsc / Geo / Econ / Hsc / Agr / Cmp / Com / Bst: D+	Chemolingot, Chwele, Imenti, Isiolo, Kapenguria, Kapkatet, Kaptumo, Kitui, Kuria, Lamu, Loitokitok, Lugari, Makueni - Mbuvo Satellite, Manza, Mbooni, Meru - Maua Satellite, Molo, Msambweni, Muranga, Ndihiwa, Nyamache, Othaya, Rachuonyo, Rera, Siaya, Tana River, Teso, Ugenya, Voi, Webuye, Narok, Muranga - Kangema Satellite, Marsabit
5.	Certificate in Community Health Assistant	Minimum Mean Grade: C- Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: D+ Bio / Bsc: D Mat A / Phy / Che / Psc / Hsc / Agr: D	Chemolingot, Imenti, Isiolo, Iten, Kabarnet, Kakamega, Kangundo, Kapenguria, Kuria, Kwale, Lodwar, Lugari, Makindu, Makueni - Mbuvo Satellite, Mander, Manza, Mbooni, Meru - Maua Satellite, Migori - Awendo Satellite, Mosoriot, Mwingi, Nairobi, Ndihiwa, Nyahururu, Nyamache, Nyandarua - Kinangop Satellite, Othaya, Rachuonyo, Rera, Shianda - Mumias, Siaya - Ugunja Satellite, Sigowet, Tana River, Taveta, Teso, Trans-Mara, Ugenya, Vihiga, Webuye, Kakamega - Navakholo, Kitui - Mutomo, Muranga - Kangema Satellite, Marsabit
6.	Certificate in Nutrition and Dietetics	Minimum Mean Grade: D+ Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: D+ Bio / Bsc: D Che / Psc: D Mat A / Phy / Gsc / Hsc / Agr: D	Chwele, Homa Bay, Kapenguria, Kwale, Lodwar, Makueni - Mbuvo Satellite, Molo, Nyandarua, Rera
7.	Diploma in Public Health	Minimum Mean Grade: C Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: C Bio / Bsc: C Mat A: C- Phy / Che / Psc: C-	Embu, Kakamega, Karuri, Kisumu, Kitui, Lake Victoria, Nyeri
8.	Certificate in Public Health	Minimum Mean Grade: C- Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: C- Bio / Bsc: C- Mat A: D	Embu, Kabarnet, Kakamega, Karuri, Kitui, Kuria, Kwale, Lake Victoria, Lugari, Manza, Nakuru, Nyeri, Othaya, Taveta, Trans-Mara
9.	Certificate in Medical Emergency Technician	Minimum Mean Grade: C -	Garissa, Gatundu, Iten, Kapenguria, Kaptumo, Machakos, Makindu, Mathare, Muranga, Mwingi, Nyeri, Port Reitz, Rera, Taveta, Thika, Voi, Kakamega - Navakholo, Muranga - Kangema Satellite
10.	Diploma in Community Health	Minimum Mean Grade: C Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: C- Bio / Bsc: D+ Mat A / Phy / Che / Psc / Hsc / Agr: D	Imenti, Isiolo, Kapenguria, Kuria, Makindu, Mosoriot, Ndihiwa, Nyahururu, Nyamache, Rachuonyo, Sigowet, Taveta, Webuye, Kakamega - Navakholo, Kitui - Mutomo
11.	Diploma in Nutrition and Dietetics	Minimum Mean Grade: C- Minimum Subject Requirements: Eng / Kis : D+ Bio / Bsc : D+ Che / Psc : D+ Mat A / Phy / Psc / Gsc / Hsc / Agr: D	Lodwar, Nyandarua
12.	Diploma in Health Counselling	Minimum Mean Grade: C Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: C Bio / Bsc: D+ Hag / CRE / IRE / HRE: C-	Makueni
13.	Diploma in Medical Engineering	Minimum Mean Grade: C Minimum Subject Requirements: Eng / Kis : C Mat A : C- Phy / Psc : C- Bio / Che / Bsc / Mw / Ect / Drd : D+	Meru
14.	Diploma in Health Promotion	Minimum Mean Grade: C Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: C Bio / Bsc: C- Mat A / Phy / Che / Psc: D+	Nyahururu
15.	Diploma in Physiotherapy	Minimum Mean Grade: C Minimum Subject Requirements: Eng / Kis: C Bio : C- Mat A / Phy / Che / Psc: C- Mat A / Phy / Che / Psc: C-	Nyeri, Port Reitz

Application Support

KUCCPS and KMTc officers will be available in all the KMTc campuses from **22nd to 27th July 2024** to assist students to submit applications.

Guidance can also be sought at the KUCCPS offices located at ACK Garden House, 1st Ngong Avenue in Community, Nairobi or all Huduma Centres. Contacts

For more information, call the KUCCPS contact centre through the numbers **0205137400 / 0723954927** or please visit KUCCPS website www.kuccps.ac.ke.

CHIEF EXECUTIVE OFFICER



Afueni kwa wakazi wa Kirinyaga mradi wa maji ukifunguliwa

NA MUTAI KIPNGETICH
(KNA)

Takriban wakazi 400,000 wa Kaunti ya Kirinyaga sasa watafurahia usambazaji wa maji safi kwa uthabiti kufuatia kutekelezwa kwa Mradi mpya wa Maji wa Kerugoya-Kutus.

Mradi huo, ambao hutoa maji yake kutoka Mito Kirinya na Thiba, umeongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 10,000 hadi mita za ujazo 30,000 kwa siku, na hivyo kumaliza mgao wa kudumu wa maji na uhaba katika maeneo mengi ya kaunti.

Mradi huu, uliotekele-

zwa kupitia juhudi za ushirikiano kati ya serikali ya kitaifa na kaunti, ni hatua muhimu katika kutoa ufikiaji wa maji safi na bei nafuu kwa wote katika kaunti.

Miji ambayo inanufaika na mradi huo ni pamoja na Kagumo, Kagio, Kerugoya, Sagana, Makutano, Kandongu, Kangai, na Mutithi. Pia kuna mipango ya kuupanua kuhudumia wakazi wa Gichugu ya juu, zikiwemo wadi za Karumandi, Baragwi, Kabare, na Njukiini.

Mradi huo unaosimamiwa na serikali ya kaunti kupitia Kampuni ya Maji na Usafi wa Mazingira ya

Kirinyaga (KIRIWASCO), umewezesha huduma endelevu ya saa 24 kutoka kwa huduma ya awali ya saa 18, hivyo basi kupunguza uhaba wa maji na mgao.

Waziri wa Kaunti anayeshughulikia Mazingira, Maji na Unyunyuzaji, James Kinyua amebainisha kuwa kutokana na ziada ya mita za ujazo 20,000 za maji zinazozalishwa kwa siku, huduma za maji sasa zitasambazwa katika maeneo ambayo hayana huduma.

“Kiwanda cha kuweka maji dawa cha mradi huko Muratiri pia kimeweza kupunguza uchafu



Mradi wa Maji kwa Wingi wa Kerugoya-Kutus Kirinyaga

wa maji na tunaweza kuwahakikishia wakazi wetu kwamba ubora wa maji umeboreshwa sana na unaweza kutumia kutoka bomba hadi mdomo.

Tunafanya upimaji wa kila mwezi ili kuhakikisha ubora unadumishwa,” akasema, akibainisha kuwa maji safi yatapunguza pakubwa kuenea

kwa magonjwa yanayotokana na maji na kuwa na athari chanya katika viwango vya kijamii na kiuchumi vya kaunti.

Mbali na kuimarisha uzalishaji na usambazaji wa maji, mradi huo ume-shughulikia kwa kiasi kikubwa kupotea kwa maji wakati wa usambazaji na hivyo kupunguza maji yasiyo ya mapato na hivyo basi kuongeza mapato ya kaunti. Wakazi wameusifu mradi huo kama “suluhisho lililosubiriwa kwa muda mrefu la matatizo ya maji katika kaunti” kwa vile sasa wanafurahia maji safi ambayo ni muhimu kwa afya zao.

Viwanda vya kahawa Nyeri kunufaika na vikaushio vipya vya sola ili kupunguza gharama

NA SAMUEL MAINA(KNA)

Kiwanda cha Kahawa cha Chorong’i katika Wadi ya Ruring’u, Kaunti Ndogo ya Nyeri ya Kati, ni miongoni mwa viwanda vinavyonufaika na vikaushio vipya vya kawi ya juu vilivyonunuliwa ili kusaidia kupunguza gharama za uendeshaji.

Mpango huo, unaoongozwa na Idara ya Mabadiliko ya Tabianchi, ni sehemu ya mpango wa Financing Locally Led Climate Action (FL-LoCA).

Mradi huo pia unazingatia Sheria ya Kitaifa ya Mabadiliko ya Tabianchi ya 2016, ambayo inaziamuru kaunti kujumuisha shughuli za mabadiliko ya hali ya hewa katika programu zao za maendeleo na miundo ya usimamizi.

Vikaushio vitaongeza uwezo wa usindikaji na ubora wa kahawa inayozalishwa na viwanda vilivyolengwa. Mkurugenzi wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Kaunti ya Nyeri Yvonne Mathenge alisema serikali ya kaunti hiyo inatarajia kuendeleza mpango huo kwa angalau viwanda vingine vinne katika siku zijazo.

“Tulikua na bajeti ya kuweka mitambo ya kukaushia jua tatu au nne na tayari tumekamilisha mbili. Tunajiandaa kuweka moja au mbili zaidi katika maeneo mengine. Ni mojawapo ya hatua za kipaumbele tunazochukua katika hatua za hali ya hewa na ubore-



Mkurugenzi wa Mabadiliko ya Tabianchi Kaunti ya Nyeri Yvonne Mathenge (mwenye kilele cha rangi ya hudhurungi) akiwa na maafisa wengine wa serikali ya kaunti hiyo walipotembelea kiwanda cha kukaushia kahawa kwa kutumia nishati ya jua cha Chorong’i katika wadi ya Ruring’u, Kaunti Ndogo ya Nyeri hivi majuzi. Serikali ya kaunti inapanga kuweka vikaushio hivyo katika viwanda vingine vinne vya kahawa katika kaunti nyingine ndogo ili kusaidia kupunguza gharama za kawi kwa hisani ya Financing Locally-Led Climate Action (FLLoCA), Picha kwa Hisani.

shaji wa uzalishaji katika sekta ya kilimo na viwanda,” aliiambia KNA.

Faida moja ya vikaushio vya sola kuliko zile za kawaida, ambazo zinatategemea jua asilia au umeme, ni kwamba za kwanza haziathiriwi na mabadiliko ya hali ya hewa au kukatika kwa umeme bila kutarajiwa.

Zaidi ya hayo, halijoto ya vikaushio inaweza kudhibitiwa kila mara ili kuepuka joto kupita kiasi ambalo linaweza kuathiri ubora wa mazao.

Bi Mathenge alisema mradi huo sio tu unakuza mbinu endelevu kwa kutumia kawi

Tunatumai upunguzaji wa mabadiliko ya tabianchi hautahusisha tu utegemezi wa usaidizi kutoka nje

ya jua bali pia unasaidia wakulima katika kupunguza gharama za usindikaji na kuongeza mapato yao.

Vikaushio vya sola vile vile vitasaidia kuboresha mchakato wa ukaushaji, na hivyo kuhifadhi ubora wa kahawa na thamani ya juu ya soko la bidhaa hiyo.

“Tunahimiza vikaushio vya sola kwa sababu mwisho wa siku ina maana wanaochoa gharama za uendeshaji na ni faida kwao (wakulima). Kwa hivyo, ni jambo zuri na linarahisisha kazi kwa sababu wana uwezo wa kuchakata zaidi, kutumia muda mchache na kutumia gharama ndogo,” aliongeza.

Mwaka jana, Idara ya Maji, Mazingira na Mabadiliko ya Hali ya Hewa ya Kaunti ilitoa pendekezo ambalo lingefanya kaunti hiyo kutenga asilimia ya bajeti yake ya maendeleo ya kila mwaka kukabiliana

na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mapendekezo hayo yamo katika Sheria ya Mabadiliko ya Tabianchi na Kanuni za Hazina ya Mabadiliko ya Tabianchi.

Hatua hiyo ilikuwa mojawapo ya hatua za kwanza katika kuhakikisha kaunti hiyo ina uwezo wa kufadhili mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

“Sheria ya Mabadiliko ya Tabianchi na Kanuni za Hazina ya Mabadiliko ya Tabianchi zinapendekeza kwamba angalau asilimia moja ya bajeti ya maendeleo ya kaunti itengwe kwa mikakati ya mabadiliko ya hali ya hewa.

“Mtindo huo utakuwa sawa na mpango jumishi wa maendeleo wa kaunti ambapo serikali ya kaunti huweka fedha katika bajeti ili kuelekea mipango hiyo,” alisema Bi Mathenge kuhusiana na udhibiti huo mpya.

IGAD yapatia Red Cross Sh20m kusaidia waathiriwa wa mafuriko

NASADIK HASSAN(KNA)

Mamlaka ya Maendeleo ya Kiserikali (IGAD) imetoa msaada wa kifedha wa Sh20 milioni kwa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini (KRCS) ili kuimarisha huduma za afya kwa jamii zilizoathiriwa na mafuriko.

Mnamo Aprili, nchi ilikumbwa na mafuriko makubwa ambayo yalisababisha uharibifu mkubwa, na kusababisha vifo vya zaidi ya 200, kujeruhi wengi, hasara kubwa ya mali na uharibifu wa miundombinu.

Katika hotuba ili-yotolewa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Utawala na Fedha, Josephat Onyari, katika hoteli moja ya Mombasa, Mkurugenzi Mtendaji wa IGAD Dkt Workneh Gebeyehu alibainisha kuwa mafuriko ya hivi majuzi yamesababisha zaidi ya watu 300,000 kuyahama makazi yao, kuharibu nyumba 10,000, na kutatiza huduma muhimu. ikiwa ni pamoja na huduma za afya.

“Maafa haya makubwa yanahitaji hatua za haraka na madhubuti. IGAD, kwa ushirikiano na washirika wetu, inatambua hitaji la dharura la kushughulikia changamoto za afya zinazokabili jamii zilizoathirika,” Dkt Gebeyehu alisema.

Msaada huo uliwezekana kupitia michango ya nchi wanachama wa IGAD ambazo ni Djibouti, Ethiopia, Kenya, Somalia, Sudan na Uganda na washirika wa maendeleo kujenga upya na kuimarisha mifumo ya afya katika kaunti zilizoathiriwa na

mafuriko.

Dkt Geneyehu alipongeza Shirika la Msalaba Mwekundu kwa kujitolea na ufansi wake katika kukabiliana na majanga ya kibinadamu kote nchini.

“Katika mwaka uliopita, liametoa msaada wa dharura kwa zaidi ya watu milioni moja, wakionyesha uwezo wao wa kukusanya rasilimali kwa haraka na kwa ufansi,” Dk Gebeyehu alisema.

“Vitendo vyao vya huruma vimewasilisha huduma ya matibabu ya kuokoa maisha, makazi, maji safi na chakula kwa wale wanaohitaji sana, ikionyesha roho ya mshikamano na huduma ya kibinadamu,” aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji alipongeza Shirika la Msalaba Mwekundu kwa kuanzisha kliniki za muda zaidi ya 50, kusambaza vifaa vya usafi zaidi ya 100,000, na kuhakikisha maji safi na usafi wa mazingira kwa watu 200,000.

“Mchango huo ni zaidi ya shughuli za kifedha; ni ushuhuda wa dhamira yetu ya pamoja kwa ubinadamu.

Inaonyesha imani yetu kwamba hakuna jamii inapaswa kuachwa nyuma, hasa wakati wa shida,” Dk Geneyehu alisema.

Aliongeza kuwa msaada huo pia unasisitiza kujitolea kwa IGAD katika kuimarisha mifumo ya afya na kujenga jamii zenye uwezo wa kuhimili changamoto za siku zijazo.

Kwa upande wake, Katiibu Mkuu wa Msalaba Mwekundu Dk Ahmed Id-riss alisema eneo la IGAD limekumbwa na hali ya dharura katika siku za hivi karibuni.

Mikataba ya wafanyikazi na Ulaya na Uarabuni kufungua ajira kwa Wakenya ng'ambo

NA CHRIS MAHANDARA(KNA)

Serikali inafuatilia makubaliano kumi na tisa ya ajira ya pande mbili na mataifa ya Ulaya Magharibi na Mashariki ya Kati ili kuwasaidia Wakenya walio na ujuzi kupata kazi nje ya nchi.

Katibu wa Idara ya Kazi na Maendeleo ya Ujuzi, Shadrack Mwadime, alieleza kuwa mazungumzo na nchi mbalimbali katika maeneo haya miwili yako katika hatua ya juu, huku serikali ikijitahidi kukabiliana na ongezeko la ukosefu wa ajira nchini.

Mwadime alisema kuwa Serikali imemaliza mazungumzo na Ujerumani, na nchi hizo mbili zimepanga

kutia saini mkataba huo Septemba mwaka huu. Hii itafungua fursa kwa Wakenya wenye ujuzi kufanya kazi nchini Ujerumani. "Tumekuwa na duru mbili za mazungumzo - moja nchini Ujerumani na nyingine hapa nchini. Ujerumani ina idadi ya watu wanaozeeka, wakati Kenya ina idadi ya vijana. Tumedhamiria kutia saini mkataba wa mahusiano ya kazi kati ya nchi hizo mbili Septemba hii ili vijana wetu waweze kupata ajira nchini Ujerumani," alisema.

Katibu alisema kuwa kupeleka Wakenya ng'ambo hakulengi tu kushughulikia ukosefu wa ajira bali pia kukuza uchumi wa Kenya kupitia pesa zinazotumwa na

watu wanaofanya kazi nje ya nchi.

Wakenya wanaoishi nje ya nchi walituma Sh663 bilioni mwaka jana. Aliongeza kuwa mpango huo wa kina wa kuunda fursa zaidi nje ya nchi unatarajiwa kuongeza kiasi hiki hadi Sh1 trilioni.

Akizungumza wakati wa Maonyesho ya Ajira Kisumu, katibu alisema makubaliano ya kazi ya pande mbili yanayofuatiliwa na serikali yanalenga kuhakikisha kuwa Wakenya wanaohamia mataifa ya kigeni hawadhulumiwi. Aliongeza kuwa wizara inashirikiana na mashirika halali ya kuajiri ili kuhakikisha kuwa Wakenya wote wanaotafuta kazi nje ya nchi wanalindwa. "Sisi hatuwapeleki nje



Katibu Mkuu wa Ukuzaji wa Leba na Ustadi (PS) Shadrack Mwadime wakati wa maonyesho ya kazi yaliyofanyika katika uwanja wa Mamlaka ya Kitaifa ya Mafunzo ya Viwanda katika kaunti ya Kisumu.

ya nchi ili mhame nchini huko kwa miaka mitatu tunataka mkafanye kazi hadi mitano mrudi ku-

wekeza nchini na kusaidia kukuza uchumi wetu," alisema.

Idara ya Serikali ya Kazi na Ukuzaji wa Ujuzi, alisema, imeanzisha zoezi la kitaifa la kutambua mapungufu katika ukuzaji wa ujuzi ili kuhakikisha kuwa wafanyikazi wa nchi wana ujuzi unaohitajika kukidhi mahitaji ya kila sekta.

Alisema kuwa mara baada ya zoezi hilo kukaamilika, litaleta mabadiliko katika mitaala ili kuhakikisha taasisi zote za elimu zinatoa wahitimu walio tayari kwa soko la ajira.

Tangu zoezi hilo lianze Februari mwaka huu, hadi sasa Wakenya 40,000 wanaotafuta nafasi za kazi wamepakia ujuzi wao kwenye tovuti ya Mamlaka ya Kitaifa ya Uajiri (NEA). Ingawa utafiti huo umetaitwaa na ukosefu wa fedha, idara ya serikali inatafuta ushirikiano na Shirika la Kitaifa ya Takwimu (KNBS) na Wizara ya Vijana ili kukamilisha zoezi hilo, katibu alisema.



MINISTRY OF INFORMATION, COMMUNICATIONS AND THE DIGITAL ECONOMY STATE DEPARTMENT OF ICT AND THE DIGITAL ECONOMY

INVITATION TO TENDER

- The Ministry of Information, communications and the Digital Economy, State Department of ICT and the Digital Economy invites tenders from eligible candidates for the provision of Operation and Maintenance of National Optic Fibre Backbone Infrastructure phase II (NOFBI II) Active and Passive Equipment lot 1 Eastern region.
- Tendering will be conducted under open tendering method using a standardized tender document. Tendering is open to all eligible and interested tenderers.
- Qualified and interested tenderers may obtain further information during office hours from **0900hrs to 1700hours** at the address given below:

**The Principal Secretary
Ministry of ICT, and the Digital Economy,
State Department for ICT and the Digital Economy
P.O BOX 30025-00200
GPO, Nairobi 8th Floor
Email: ictprocurement@information.go.ke**
- Tender documents may be viewed and obtained electronically from the Ministry's Website: www.ict.go.ke. The tender documents obtained electronically will be **free of charge**.
- A site visit for the various sites will be conducted on the dates specified in the tender document for the provision of Operation and Maintenance of National Optic Fibre backbone Infrastructure phase II (NOFBI II) Active and Passive Equipment lot 1 Eastern region
- Tenderers downloading documents from the designated website shall advise the procurement Entity that they have downloaded the tender documents, giving full contact address of the tenderers to ictprocurement@information.go.ke to facilitate any further clarification or addendum.
- All tenders Must be accompanied by a Tender Security of **2%** of the total tender sum from a reputable bank registered by the Central Bank of Kenya or Insurance Company Registered by the PPRA valid for a period of **150 days**.
- The Tender validity period shall be **150 days** from the tender opening/closing date.
- The tenderer shall chronologically serialize all pages of the tender documents submitted.
- Completed tenders must be delivered to the address below on or before **6th August, 2024 at 10:00 am**

**The Principal Secretary
Ministry of ICT, and the Digital Economy,
State Department for ICT and the Digital Economy
P.O BOX 30025-00200
GPO, Nairobi
8th Floor procurement unit.**

- Tenders will be opened immediately thereafter in the presence of bidders or representatives who choose to attend the tender opening process in the 9th floors boardroom at Telposta Towers.
- Late tenders will be rejected.**
- The Government reserves the right to reject any tender giving reasons for the rejection.

PRINCIPAL SECRETARY
Ministry of ICT, and the Digital Economy,
State Department for ICT and the Digital Economy



ENGINEERS BOARD OF KENYA

GRADUATE ENGINEERS INTERNSHIP PROGRAM

INTERNSHIP OPPORTUNITIES

The Engineers Board of Kenya (EBK) is a statutory body established under Section 3(1) of the Engineers Act, 2011. The Board is responsible for the registration of engineers and engineering firms, regulation of engineering professional services, setting of standards, development and general practice of engineering.

One of the functions of the Board under the Engineers Act, 2011 Section 7 (1) (q) is to plan, arrange, coordinate and oversee continuing professional training and development and facilitate internship of graduate engineers.

The Engineers Board of Kenya has developed Graduate Engineers Internship Program (GEIP) which is a structured internship program for graduate engineers that is designed to enable them to acquire requisite hands-on skills and prepare them for professional practice in their respective engineering fields.

The program will run for 36 months, and the interns will be trained under professional engineers who are registered by the Board.

Qualifications for the Graduate Engineers Internship Program

The Board is seeking to provide internship opportunities to those candidates who:

- Are registered graduate engineer by EBK within the last two years
- Are available for the entire duration of the internship
- Are **NOT** in any form of employment

The Engineers Board of Kenya is committed to diversity and gender equality and therefore encourages persons living with disability, women and those from marginalized areas to apply.

Please Note

- The deadline for application is **Friday 9th August 2024 at 5pm EAT**
- The Board does not guarantee employment after completion of the Internship Program
- The Board **DOES NOT** charge any fee for this process.
- Only successful applicants will be contacted.
- Successful applicants will be expected to provide the following additional information/documents:

- A valid personal accident insurance cover
- A valid personal medical insurance cover by NHIF or any other reputable medical insurance firm
- Certificate of Good Conduct
- Clearance from Ethics and Anti- Corruption Commission (EACC)
- Kenya Revenue Authority PIN Certificate

- Any form of canvassing will lead to automatic disqualification.
- All applications **MUST** be submitted online via the procedure below.

Application Procedure

- Log on to www.ebk.go.ke
- Click on the Training and Development tab
- Click on the Graduate Engineers Internship Program, then click on **"Apply to Graduate Engineers Internship Program"**
- "Sign up" to create an account then submit your application.

In case of any challenge or issues, please send an email query to registrar@ebk.go.ke or call **0722 509 972**.



Chidzuga ahimiza wakazi wa Kwale kukumbatia kazi kutoka kwa miradi

NA MUNIRA MANDANO (PCO)

Naibu Msemaji wa Serikali, Mwanaisa Chidzuga, amewataka wakazi wa Kwale kutumia vyema fursa zinazotolewa na miradi na mipango ya serikali katika eneo hilo ili kujimarisha na kujikimu kimaisha.

Akizungumza katika maeneo bunge ya Matuga, Kinango, Msambweni, na Lungalunga, Chidzuga alisema kuwa mradi wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu katika mji wa Kwale na ujenzi unaoendelea wa chuo cha baharini katika eneo la Chitsakamatsa katika Wadi ya Waa, miongoni mwa mingine, unaweza kubuni fursa za ajira kwa wakazi.

“Miradi hii yote ya serikali ya kitaifa ni nafasi za kazi kwenu. Nendeni mkaajiriwe katika miradi hii, na mtapata riziki kutoka kwayo,” alisema.

Pia aliwahimiza wanawake kuuza vyakula vilivyopikwa kwenye maeneo ya ujenzi jambo ambalo pia litakuza bi-



ashara zao.

“Kwa mama zetu ambao hawawezi kuajiriwa katika maeneo ya ujenzi, mnaweza kuwauzia watu wanaofanya kazi katika maeneo ya ujenzi chakula kilichopikwa na hilo litakuza biashara zenu,” Chidzuga alisema.

Alisema makundi ya vijana na wanawake yanafaa kujisajili kama makampuni ili kupata zabuni za biashara kutoka kwa serikali ya kaunti na ya kitaifa. “Tuna wanawake wengi katika vikundi na vijana ambao wanachangishiana pesa, tafadhali sajili vikundi hivi kama

kampuni na muombe zabuni kutoka kwa serikali. Maombi yako yatazingatiwa kwa zabuni hizi, na mtajiendelea,” alisema.

Chidzuga alibainisha kuwa serikali pia ina mipango tofauti kama Inua Jamii, Hazina ya Hustler, Hazina ya Biashara ya Wanawake miongoni mwa zingine ambazo zote zimewekwa kusaidia Wakenya kuwezesha na kukuza biashara zao.

“Fedha hizi zipo kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara na wanawake na hata vijana wanapaswa kuomba fedha hizi ili kujiwezesha,” alisema.

Mahakama yahakikishia wafanyabiashara ubora, haki ya kibiashara yenye ufanisi

NA JOSEPH NG'ANG'A (KNA).

Idara ya Mahakama inajenga imani katika mfumo wake wa haki za kibiashara ili kuimarisha mazingira ya biashara na kuhimiza ongezeko la uwekezaji nchini Kenya kwa kuhakikisha ubora na uadilifu wa haki ya kibiashara.

Jaji Mkuu Martha Koome alisema kuwa mwongozo wa kimkakati wa kitaasisi, ‘Mabadiliko ya Kijamii kupitia Upatikanaji wa Haki (STAJ),’ unatambua jukumu muhimu la Mahakama katika kuwezesha mazingira mazuri ya kiuchumi.

“Kwa kuhakikisha utatuzi wa migogoro kwa gharama nafuu na unaoafaa, tumejitolea kuimarisha urahisi wa kufanya biashara katika nchi yetu,” Koome alisema.

Akizungumza katika hoteli moja ya Nairobi wakati wa Mkutano na Muungano wa Sekta ya Kibinafsi Kenya (KEPSA), Jaji Mkuu Koome alisisitiza kuwa mkutano huo wa kila mwaka unaaangazia kuwa Idara ya Mahakama kutambua jukumu kuu linalotekelezwa na washikadau katika kuimarisha ufanisi wa mfumo wa mahakama.

Koome alisema ushirikishaji huo ulikuwa muhimu kwa kuwa uliwasaidia kuunda ushirikiano wa kimkakati unaoenga kuimarisha ufanisi wa mfumo wa mahakama.

Jaji Mkuu alieleza kuwa Idara ya Mahakama imepata maendeleo makubwa kuhusu uwekaji kumbukumbu na uwekaji mitambo ya dijitali, akisema kuwa katika mwaka uliopita, wamefaulu

kusambaza mfumo wa uhifadhi wa faili mtandaoni kote nchini tangu Machi 2024 baada ya majaribio ya awali katika Kaunti ya Jiji la Nairobi kuanzia Julai 2020.

“Tangu Machi 2024, kesi zote na hati nyingine za mahakama sasa zimewasilishwa mtandaoni katika vituo vyetu vyote vya mahakama kote nchini,” alisema.

Koome aliongeza kuwa jukwaa la ufunguaji faili mtandaoni huruhusu kesi kuwasilishwa kidijitali, hivyo basi kuondoa hitaji la kuhudhuria mahakamani kwa walalamishi na mawakili. Pia inasaidia tathmini ya ada za mahakama, kufuatilia mtandaoni hali ya kesi, kutegea maafisa wa mahakama kesi kwa njia ya dijitali, na upakuaji kwa urahisi wa hati za kesi. “Majaji na mahakimu wanaweza kuandaa, kuhariri, na kuchapisha maamuzi, hukumu na magizo mtandaoni, na pia kutoa takwimu za kesi ya mtu binafsi na ripoti za utendakazi kupitia Mahakama ya kufuatilia kesi inayokabili sehemu ya mfumo wa kielektroniki,” Koome alisema.

Jaji Mkuu alisema kupitia mfumo wa kielektroniki, Mahakama inakuza utangamano na ushirikiano wa mifumo ya habari na mashirika mengine ya sekta ya haki. Mfumo huo tayari umeunganishwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, na juhudi zinaendelea kujumuisha mashirika mengine.

“Mahakama inazindua mfumo unaoendeshwa na Akili Unde ili kusaidia katika kutoa usaidizi kwa vituo kadhaa vya mahakama kukiwa na mipango ya kupanua nchi nzima kupitia kuanzishwa kwa Kituo cha Unukuzi cha Mahakama

Gavana ahimiza wakazi kujiandikisha kwa mpango nafuu wa huduma za afya

NA RENNISH OKONG'O (KNA)

Gavana wa Kaunti ya Elgeyo Marakwet Wisley Rotich ametangaza lengo lake la kila familia katika kaunti hiyo kusajiliwa na Mamlaka ya Afya ya Kijamii (SHA) kufikia Desemba 2024.

Hatua hii inanuiwa kuhakikisha kuwa wakazi wote wananufaika na mpango huo na kupunguza hafla za kuchangisha pesa, zinazojulikana kama harambe, ili kulipia gharama za afya. Akizungumza wakati wa uzinduzi usajili wa SHA katika Moi Girls Kapsowar katika Kaunti Ndogo ya Marakwet Magharibi, Gavana Rotich alieleza kuridhishwa kwake na mbinu jumuishi na ya bei nafuu ya SHA kwa huduma za afya.

“Nina furaha kwamba Mamlaka ya Huduma ya Afya ya Jamii inachukua tathmini ya kila mtu na inakidhi mahitaji ya kila mtu binafsi kwa kuwa ni nafuu,” alisema.

Gavana Rotich aliangazia ugumu wa kifedha unaotokana na bili kali za afya, ambazo mara nyingi huingiza familia katika umaskini. “Wengi wanalazimika kuuza ardhii yao ili kufidia bili kubwa, haswa katika visa ambavyo mwanafamilia anagunduliwa na saratani,” alibainisha. Alisisitiza uwezo wa kumudu mpango huo, akisema,



Dkt Patrick Amoth, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Afya, wa pili kulia, Gavana wa Kaunti ya Elgeyo Marakwet Wisley Rotich akijiandikisha kwa SHA jana katika uwanja wa Moi Kapsowar Girls huko Elgeyo Marakwet.

“Unalipa mia tatu yako, na iliyobaki itatuliwa ikiwa unahitaji msaada.” Gavana pia alitaja faida kubwa katika afya ya msingi.

“Jambo zuri zaidi ni kwamba katika zahanati na vituo vya afya, huduma zitakuwa bure kwani pesa za huduma ya afya ya msingi zitapelekwa hospitalini. Ili hili lifanyike ni lazima uandikishwe,” aliongeza.

Dkt Patrick Amoth, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Afya, aliunga mkono maoni ya Gavana Rotich, akisisitiza mabadiliko ya SHA kwenye mfumo wa afya wa Kenya.

“Huduma tunazozizindua leo zitaimarisha idara ya afya na kuimarisha maisha ya Wakenya kwa kuzingatia sheria,”

Dkt Amoth alisema, akiangazia mfumo wa kisheria unaounga mkono mpango huo.

Aliwataka washirika muhimu, wadau, walimu, viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini na vijana kuungana mkono katika mpango huu.

“Tunahitaji kutembea pamoja safari hii ili tuweze kufanikiwa kama nchi,” alisema.

Dkt Amoth pia alisisitiza umuhimu wa dhamira ya kisiasa kufikia bima ya afya kwa wote.

“Kiungo kikubwa kinachohitajika kwa nchi duniani kote kuweza kufikia huduma ya afya kwa wote ni kuelimika kisiasa, kama Rais alivyoonyesha. Kwa hiyo, kushindwa si chaguo tunapoendelea katika safari hii,” alihitimisha.

Wanawake wa Laikipia wapokea matangi 50 ya maji kudhibiti ukame

NA MUTURI MWANGI (KNA).

Wanawake wafugaji katika Kaunti Ndogo ya Laikipia Kaskazini wamenufaika na matangi ya maji ili kuhifadhi maji wakati wa mvua inayoendelea, hatua inayolenga kuwaepusha na ukame wa kudumu.

Matangi hayo 50 ya maji kila moja likiwa na ujazo wa lita 3,000, yalitolewa na shirika la Habitat for Humanity Kenya kwa ushirikiano na serikali ya Kaunti ya Laikipia na kusambazwa kwa vikundi vya wanawake katika maeneo ya Naibor na Kiandutura, ambayo huathirika zaidi na hali ya hewa kavu.

“Tangi hili litaongeza uwezo wangu wa kuhifadhi maji, kuhakikisha maji yanatosha kwa matumizi ya nyumbani na mifugo. Wakati huo huo, litanisaidia kujikita katika shughuli nyingine bila kuhangaikia maji,” alisema Zipporah Lang’at, mmoja wa walionufaika wakati wa zoezi la kukabidhiwa huko Naibor, wadi ya Segera.

Aidha alifichua kuwa hapo awali alitumia muda wake

mwingi kuchota maji jambo ambalo lilimnyima fursa ya kujishughulisha na shughuli nyingine za kujikimu kimaisha.

Mkurugenzi wa mpango wa Habitat for Humanity Kenya Nixon Otieno alisema wana nia ya kusaidia wanawake wafugaji ili kupata mapato kupitia kilimo na shughuli msoto za maisha. Zaidi ya hayo, alidokeza kuwa mpango huo unaendana na ajenda ya serikali ya kuongeza uzalishaji wa kilimo kupitia teknolojia ya kilimo kinachozingatia hali ya hewa. Karani wa Kaunti ya Laikipia Koinange Wahome alipongeza mpango huo aki-bainisha kuwa utaboresha upatikanaji wa maji katika kaunti hiyo jambo ambalo bado ni changamoto hasa nyakati za kiangazi.

“Nimefurahi kwamba kupitia ushirikiano huu, tunapiga hatua katika kutatua changamoto za maji. Juhudi hizi zinaendana na maono yetu ya kusambaza matangi 50,000 ya maji ifikapo 2027 kwa wakazi,” alisema Wahome.

Mradi mpya wa KALRO kuzalisha tani 5.8 za mbegu za mpunga unakomaa haraka

NA WANGARI NDIRANGU (KNA)

Shirika la Utafiti wa Mifugo na Kilimo Kenya (KALRO) limezindua uundaji wa mfumo endelevu wa uzalishaji wa mbegu za mpunga ulio-dhinishwa ambao unatarajiwa kubadilisha maisha ya wakulima kwa kutoa mbegu za mpunga iliyo-dhinishwa kwa bei nafuu ili kuboresha uzalishaji.

Kupitia mradi wa miaka mitano wa Ushirikiano na Korea kwa Kilimo Bunifu (KOPIA), KALRO itasaidia uzalishaji wa mbegu zinazokomaa haraka, kuongeza mbegu bor goa zilizoidhinishwa na usambazaji wa mbegu zilizoidhinishwa za mpunga kwa wakulima wa mpunga.

Akizungumza mjini Mwea wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa KALRO Dkt Eliud Kireger alisema sekta ya mpunga nchini Kenya haijakidhi ongezeko la mahitaji ya mchele. Suala hili limechangiwa na kuongezeka kwa watu



KALRO- KOPIA aina ya mbegu ya Komboka.

wa tabaka la kati na kukua kwa miji, huku watu wengi wakitegemea mchele kwa chakula.

“Matumizi ya mchele nchini yanapanda hasa kwa sababu ya vijana wanaoacha ‘ugali’ na m kutumia mchele. Idadi ya watu mjini nchini Kenya pia inakadiriwa kufikia asilimia 50 ya watu wote ifikapo mwaka 2050, ambayo ina maana kwamba mahitaji yao ya chakula yatasababisha upungufu mkubwa

wa mchele,” alisema.

Mkurugenzi Mkuu alieleza kuwa kwa sasa, mahitaji ya mchele kwa mtu mmoja kwa mwaka ni kilo 28 lakini, kwa kuangalia mwenendo wa sasa, Wakenya wanatarajiwa kutumia takriban kilo 30 za mchele kwa kila mwananchi ifikapo 2027 ikiwa ni jumla ya tani milioni 1.8 za mchele.

“Kwa sasa tunatumia takriban tani 950,000 hadi milioni moja za mchele

ambapo tunazalisha tani 200,000 tu, upungufu wa asilimia 80 na ili tuweze kuziba pengo hilo, tunahitaji kuwa na mfumo wa mbegu ambao unatuhakikishia mbegu bora za bei nafuu, ili wakulima waweze kuongeza uzalishaji,” alisema.

Alieleza kuwa ili kuki-dhi mahitaji hayo, serikali kupitia Agenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi kuanzia mashinani ‘nguzo ya kupunguza uagizaji bidhaa kutoka nje’, inalenga kuwa na kasi ya ukuaji wa mwaka ya asilimia 25 katika uzalishaji wa mpunga.

“Tunatumia katika miaka minne hadi mitano ijayo, tutakuwa tumeziba pengo hilo kwa asilimia 50 hadi 60 ya kile tunachozalisha, na hii itafanywa kwa kuboresha upatikanaji wa mbegu zilizoidhinishwa sokoni kwa mazao ya juu,” aliongeza.

Dkt Kireger alisema kuwa katika mfumo wowote wa uzalishaji wa mazao, umuhimu wa ubora wa mbegu na mifumo bora ya mbegu hauwezi kupuuzwa.

KWA UFUPI

Bodi yaonya umma kuhusu dawa bandia za kisukari

Bodi ya Kuthibiti Dawa na Sumu (PPB) imetahadharisha umma kuhusu dawa feki za ugonjwa wa kisukari, ikiwataka wagonjwa kuwa makini na kutoa taarifa kwa yeyote anayeuza dawa zinazotiliwa shaka. Afisa Mkuu Mtendaji wa PPB Dkt Fred Siyoi alisema Bodi ilipokea tahadhari kutoka kwa Interpol kuhusu dawa feki za Ozempic pens (semaglutide). Apidra Solostar pens (glulisine), zinazotumiwa kutibu kisukari aina ya 1 na aina ya 2, zimepewa jina la Ozempic (semaglutide) pens.

“Kwa hivyo, Bodi ingependa kufahamisha umma kwamba Ozempic pens kwa sasa hazijasajiliwa au kuidhinishwa na Bodi kuuzwa Kenya.

Kwa hivyo, bidhaa yoyote inayouzwa kama Ozempic pens ni kinyume cha sheria, na Bodi haiwezi kuthibitisha usalama, ubora na ufanisi wake,” Dkt Siyoi alieleza.

Ili kulinda usalama wa umma, alisema Bodi imechukua hatua za haraka

na kuongeza ufuatiliaji ili kuthibitisha kama Ozempic pens feki zinazauza katika Kenya kwa sasa.

“Bodi inatahadharisha umma na wataalamu wa afya dhidi ya biashara, usambazaji, uuzaji wa jumla, reja reja, kutoa, kusambaza, matumizi au usimamizi wa wagonjwa wa Ozempic pens, kwa kuwa vitendo kama hivyo ni haramu na vinahatarisha afya na usalama wa umma,” Afisa Mkuu Mtendaji alisema.

Alitoa wito kwa umma na wataalamu wa afya kutoa mara moja taarifa zozote kuhusu Ozempic pens kwa Bodi ya Dawa na Sumu. Alieleza kwamba ripoti hizo zinaweza kutolewa kwa kituo cha huduma za afya kilicho karibu au kwa Bodi ya Dawa na Sumu kupitia tovuti yao <https://pv.pharmacyboardkenya.org/users/mpublic>; Programu ya simu ya mkononi: mPVERS, USSD *271#, barua pepe: pms@ppb.go.ke au Nambari ya Simu 0795743049

Judy Sheri and Joseph Ng'ang'a

Matumaini ya timu ya Kenya Olimpiki kung'aa Paris 2024

Katibu wa Michezo Mhandisi Peter Tum ana matumaini kuwa timu ya Kenya italeta angalau medali nane za dhahabu kutoka Michezo ya Olimpiki ya Paris 2024.

Mhandisi Tum alikuwa akizungumza katika afisi ya Wizara katika Talanta Plaza huku Kamati ya Kitaifa ya Olimpiki ya Kenya (NOCK) ikitangaza hadharani orodha ya mwisho ya kikosi cha Kenya katika michezo hiyo.

Matokeo bora ya Kenya katika historia ya Michezo ya Olimpiki yalikuwa mwaka wa 2008 wakati wa Michezo ya Olimpiki ya Beijing, ambapo nchi ilijizolea jumla ya medali 16: medali sita za dhahabu, medali nne za fedha na sita za shaba. “Mimi si mwanariadha, lakini nina imani timu hii italeta nyumbani angalau medali nane za dhahabu. Maandalizi yamekuwa ya hali ya juu ndani na nje ya nchi kupitia mashirikisho yao, na timu tunayoipeleka Paris ndiyo bora zaidi,” alisema Tum ambaye atakuwa mkuu wa wajumbe wa timu hiyo na kiongozi wa ngazi ya juu kabisa serikalini.

Aliongeza, “Ninataka kumshukuru Rais William Ruto kwa kuiaga timu mnamo Julai 5 na kuhakikisha kuwa marupurupu wakati huu ni ya juu sana. Aina hii ya motisha inatuhakikishia medali nyingi.”

“Kando na kushiriki Olimpiki, Kenya pia itakuwa ikijitangaza. Tutaonyesha uwezo wetu wa utalii kama kivutio bora zaidi barani Afrika, pia tutaangalia biashara, na ndio maana tumesimamia Nyumba ya Kenya huko Paris.

Timu hiyo inajumuisha wanariadha 81, maafisa wa timu 33, washiriki 26 wa timu ya usimamizi, na washiriki watano wa familia ya Olimpiki. Ni timu ndogo ikilinganishwa na kikosi kilichosafiri hadi Michezo ya Olimpiki ya Tokyo 2020.

Rais wa Nock Paul Tergat alisema wanariadha hao zaidi ya 80 watashiriki michezo tofauti, ambayo ni: riadha, raga, voliboli, judo, na kuogelea.

“Ni siku nane rasmi kabla ya michezo ya Olimpiki ya Paris, kumaanisha kwamba tuko kwenye mkondo wa mwisho wa mwaka muhimu kwa wanamichezo. Michezo inakaribia kuanza. Ni wakati wa kila mwanariadha kuingia katika hali ya kushindana.

Na Mwandishi wa MyGov

Eneo la Mlima Kenya kufaidika na mpango wa maendeleo ya maji na usafi wa Sh63b

NA WANGARI MWANGI(KNA)

Shirika la Maendeleo ya Maji la Tana (TWWDA) linatafuta Sh 63 bilioni kumimarisha usambazaji wa maji na kuboresha huduma za usafi wa mazingira katika kaunti tano za ukanda wa Mlima Kenya katika muda wa miaka mitano ijayo. Mapendekezo haya yameainishwa katika Mpango Mkakati wa 2023-2027, unaolenga kuongeza upatikanaji wa huduma bora za maji kutoka asilimia 57.8 hadi 90 ifikapo mwaka 2027. Aidha, shirika linalenga kuongeza huduma za usafi wa mazingira kutoka asilimia 8.1 hadi 30 ifikapo mwisho wa kipindi chq utekelezaji.

Ili kufikia malengo haya, TWWDA itategemea serikali kuchangia Sh 8.5 bilioni kusaidia miradi hiyo. Miradi hii itatelezwa katika kaunti za Embu, Kirinyaga, Nyeri, Tharaka-Nithi, na Meru.



Katibu Msimamizi katika Idara ya Maji na Usafi wa Mazingira, Stephen Kihara (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Tana Water Works Development Agency Mha Phillip Gichuki (Watatu Kulia) pamoja na wajumbe wa bodi ya shirika hilo wakati wa uzinduzi wa Mpango Mkakati wa shirika wa 2023-2027 kwenye Bantu Resort katika Kaunti ya Nyeri.

Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta ya Kibinafsi utachangia Sh 30 bilioni katika mpango huo huku Sh 21.7 bilioni zikipatikana kutoka kwa washirika wa maendeleo. Na Sh 3.5 bilioni zitakazobaki zitatokana na shughuli za kuzalisha mapato ndani ya shirika.

Akizungumza katika

hoteli ya Nyeri wakati wa uzinduzi wa mpango mkakati huo, Afisa Mkuu Mtendaji wa TWWDA Mhandisi Philip Gichuki alisema kuwa Shirika hilo linanuia kutekeleza miradi 32 ya maji katika azma yake ya kuongeza maji katika kaunti zote tano.

Aidha, shirika limepanga miradi 14 ya usafi wa maz-

ingira ambayo itagharimu Sh 8 bilioni kutekeleza.

“Tunalenga kufikia asilimia 90 ya upatikanaji wa maji ifikapo 2027. Mpango mkakati umeweka malengo mahususi yanayohusu kaunti mahususi. Tuna miradi mikubwa ya usambazaji maji ambayo tunataka sana kufikia idadi ya watu ndani ya kaunti hizi na maji ya kutosha. Tunapofanya miradi ya maji, tunapaswa pia kuhakikisha kuwa taka zinazozalishwa zinashughulikiwa. Kwa hivyo, tutakuwa pia na kipengele cha usimamizi wa taka,” akabainisha Mhandisi Gichuki.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa mradi wa usambazaji maji wa Sh 1.6 bilioni katika kaunti ya Embu ambao utanufaisha takriban wakazi 250,000 na mradi wa usambazaji maji kwa wingi wa Sh 1.1 bilioni wa Kirinyaga unaoenga wakazi 100,000 wa Kirinyaga Kusini Mashariki.